


SPACE SCOOP

Bringing news from across the Universe to kids all around the world



EU UNIVERSE
AWARENESS

Mbio za Nyota Angani



Hakuna kitu chochote angani ambacho kimesimama, nyota nyingi husogea kama wanariadha wa mbio ndefu ambao hawasimami hadi wafikie mastari wa mwisho, vivyo hivyo nyota huwa zimasogea huko angani ijapokuwa zenyewe hutembea maisha yao yote. Ingawa katika siku za hivi karibuni wanaastronomia wameweza kutambua nyota ambayo inafananishwa wa wakimbajji wa mbio fupi (angalia nyota iliyozungushwa katika boxi kwenye picha).

Ili kuweza kufahamu muendo kasi wa nyota hii wanaastronomia ilibidi watambue umbali iliyotembea tangu ilipoanza kusogea na kwa mda gani ilichukua kufika umbali huo. Wanaastronomia hawa wanafikiri kuwa nyota hii imeanza safari yake kutokea katiki ya wingu la gesi na vumbu linalonekana kwa rangi ya zambarau katika picha. Nyota hii ni maalum kwani inazunguka kwa haraka sana na kutohana na hivyo imejumuishiwa katika kundi la nyota zifulikanalo kama pulsar. Pulsar hii ilijiefenga na wingu la zambarau wakati wa mlipuko uliotengeneza wingu la gesi na vumbi.

Tathimini ya wanaastronomia imeonyesha kuwa pulsar hii inasogea katika mwendo kasi wa ajabu sana katiki ya kilometra millioni 9 na 11 katika lisaa limoja! Mwendo kasi huu unaweza kuifanya nyota hii kuwa na mwendo kasi kupita pulsar zote zinazojulikana hadi leo! Ingawa bado kuna utata katika kupata cheo hicho kwani kuna pulsar nyingine ambayo imekadiliwa kuna na mwendo kasi katiki ya kilometra millioni 5 na 10 lisaa limoja.

Ni jambo la kusikitisha kuwa wanaastronomia hawawezi kuzifanya nyota hizi mbili zishindane kukimbia ili kutambua ni ipi ina kasi zaidi ya mwenzake na badala yake inawabidi kukokotoa kwa umakini mahesabu yao ili kujua ipi ina mbio zaidi.

COOL FACT

Kama pulsar inasogea katika mwendo kasi wa kilometra 11 kwa saa, hii inamaanisha kuwa inaweza kusafiri kuzunguka mastari wa Equator wa sayari ya Dunia katika sekunde 13!



More information about EU-UNAWE
Space Scoop: www.eu-unawe.org/kids/